

ti ugonjwa wa mnyauko fuzari
mayuno mengi.



Kwa maelezo zaidi wasiliana na:


Mkurugenzi wa Kanda
Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Ukiriguru
S.L.P. 1433
Mwanza.

Simu: 028 2550215

Fax: 028 2550214

E-mail: ukiriguru@africaonline.co.tz

Kipeperushi hiki kimetayarishwa na
Taasisi ya Kilimo Ukiriguru na
kimefadhiliwa na Serikali ya
Tanzania.



Kipeperushi hiki hakiuzwi

ONGEZA MAVUNO YA PAMBA
KWA KUDHIBITI UGONJWA
WA MNYAUKO FUZARI



Nini maana ya mnyauko fuzari?


- Mnyauko fuzari ni ugonjwa wa pamba ambao husababisha kupungua kwa mavuno.

Ugonjwa huu husababishwa na nini?

- Husababishwa na viini aina ya ukungu.

Je unafahamu dalili za ugonjwa huu?

- Uotaji wa mbegu za pamba hupungua
- Mimea wa pamba hudumaa
- Majani hubabuka na kujikunja kwa juu kama karai
- Mimea hupukutisha majani kwa urahisi
- Shina na matawi ya mimea huvunjika kwa urahisi
- Sehemu ya ndani ya shina hubadilika rangi na kuwa nyeusi




Unafahamu ugonjwa huu unavyoenea?

- Huenea ukipanda mbegu zizizo safi zenye ugonjwa
- Ukিপanda mbegu zizozostahimili ugonjwa
- Ukitumia mabaki ya pamba yenye ugonjwa shambani
- Ukilima pamba mfululizo sehemu moja
- Usipongoa na kuchoma moto mimea yenye ugonjwa shambani

Unafahamu athari za ugonjwa huu?

- Mavuno ya pamba yatapungua zaidi ya asilimia 20
- Mapato yako na ya taifa kifedha yatapungua
- Huduma za jamii kama shule, zahanati, barabara zitapungua



Je, unazijua njia za kudhibiti ugonjwa huu?

- Tumia mbegu sai kutoka jineri
- Tumia mbegu bora zinazostahimili ugonjwa mfano UK 77; UK 91
- Ngo'a na kuchoma moto mimea ya pamba yenye ugonjwa.
- Epuka matumizi ya mabaki ya pamba yenye ugonjwa mashambani
- Tumia kilimo mjzunguko cha pamba na mhogo, mtama au mahindi
- Ngoa na kuchoma moto masalia ya pamba

Je, unazijua njia nyingine za kupata ushauri?

- Onana na bwanashamba aliye karibu na wewe

